

# Tafakari Kabla ya Kuchanja Chale

Je, umewahi kushawishiwa kuchanja chale (*tattoo*)?  
Kabla ya kufanya jambo lolote fikiria yafuatayo:

## WEWE UNAONAJE?



Una maoni gani kuhusu chale?



Zinafaa

Hazifai

Inategemea lengo  
au ujumbe

Inategemea  
mahali  
utakapoichora

Inategemea  
ukubwa wake

# TUMIA MAANDIKO KUTAFAKARI

Nataka kuchanja chale kwa sababu \_\_\_\_\_



Ni jambo la kawaida;  
kila mtu anafanya hivyo!



**Andiko:** “Na msijikatekate mwili wenu kwa ajili ya nafsi iliyokufa, wala msijitie alama ya chanjo.”—**Mambo ya Walawi 19:28.**

**KWELI AU SI KWELI:** Sheria hiyo waliyopewa Waisraeli, inawahusu Wakristo.

**Jibu:**  
**SI KWELI.**

Wakristo hawako tena chini ya Sheria ya Musa. (Waebrania 7:18-22) Hata hivyo, andiko la Mambo ya Walawi 19:28 linaonyesha maoni ya Mungu kuhusu jambo hilo. Watu waliowazunguka Waisraeli walijichora majina au alama za miungu yao.

**Unafikiri ni kwa nini Mungu aliwakataza Waisraeli wasijichanje chale?**

---

---

---

**Basi ni katika hali gani, kujichanja chale kungekuwa ni jambo lisilokubalika kabisa kwa Wakristo?**

---

---

---



Mchoro huo una ujumbe mzuri, na unanisadia kumkumbuka mtu ninayependa.

**Andiko:** “Andiko lote limeongozwa na roho ya Mungu nalo ni lenye faida kwa kufundisha, kwa kukaripia, kwa kunyoosha mambo, kwa kutia nidhamu katika uadilifu, ili mtu wa Mungu awe na uwezo kamili, akiwa na vifaa kamili kwa ajili ya kila kazi njema.”

—2 Timotheo 3:16, 17.

**Andiko:** “Lakini yeye anayechunguza ndani ya sheria kamilifu iliyo ya uhuru na ambaye hudumu katika hiyo, mtu huyo, kwa sababu amekuwa, si msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, atakuwa mwenye furaha katika kuitenda.”—Yakobo 1:25.



Je, unafikiri kwamba ujumbe unaofaa—kwa mfano, maneno au wazo la Kimaandiko—utakuwa ni alama inayokubalika?

Ndiyo, kwa sababu \_\_\_\_\_

Hapana, kwa sababu \_\_\_\_\_

Ni njia gani bora zaidi itakayokusaidia kujikumbusha sheria na kanuni za Kimaandiko?

---

---

---

Kuna njia gani nzuri zaidi ya kuwakumbuka wale tunao-wapenda?

---

---

---

“Utahisije ikiwa umempa mtu zawadi nzuri, halafu yeye anatumia wino usiofutika kuandika kila mahali kwenye zawadi hiyo? Hivyo ndiyo huenda Muumba anavyohisi tunapojichanja chale mwilini.”—Anna.



Nafikiri ni wenye kuvutia. Hata hivyo ni mchoro tu, na huu ni mwili wangu.

**Andiko:** “Na kujipamba kwenu kusiwe kule kusuka nywele kwa nje na kule kujivika mapambo ya dhahabu au kuvaa mavazi ya nje, bali kuwe yule mtu wa siri wa moyoni katika vazi lisiloharibika la roho ya utulivu na ya upole, ambayo ni ya thamani kubwa machoni pa Mungu.”—1 Petro 3:3, 4.

**Andiko:** “Yehova anataka nini kutoka kwako ila kutenda haki na kupenda fadhili na kuwa na kiasi katika kutembea na Mungu wako?” —Mika 6:8.



Unafikiri ni kwa nini katika Biblia kuwa na kiasi ni jambo lenye thamani?

---



---

### Mwonekano wako unaweza kuwaathiri wengine jinsi gani?

<b>WATU WENGINE</b> Soma 2 Wakorintho 6:3.	<b>RAFIKI ZAKO</b> Soma 1 Wakorintho 10:31-33.	<b>MUNGU WAKO</b> Soma Waroma 12:1.
Kwa nini ni muhimu kufikiria jinsi wengine wanavyokuona? <hr/> <hr/> <hr/> <hr/>	Ikiwa nitachanja chale, nitawaathiri wengine jinsi gani? <hr/> <hr/> <hr/> <hr/>	Kwa nini Mungu anajali kuhusu jinsi unavyoutendea mwili wako? <hr/> <hr/> <hr/> <hr/>